## Vipimo vya kugundua saratani mapema

Australia ina programu tatu za uchunguzi wa saratani. Programu hizi hutumia vipimo rahisi ili kupata dalili za awali za saratani ya utumbo, matiti na shingo ya kizazi. Kugundua saratani mapema hurahisisha kutibu, na uwezekano wa kuishi unakuwa ni mkubwa zaidi.

Vipimo hivyo ni kwa watu ambao hawana dalili za saratani. Ikiwa una dalili za saratani, mwambie daktari wako.

Vipimo vitatu hivyo ni vya bure ikiwa una kadi ya Medicare ya kijani au ya buluu (ya muda mfupi). Ikiwa huna kadi ya Medicare, zungumza na daktari wako kuhusu gharama ya vipimo.

### Uchunguzi wa saratani unaweza kuokoa maisha yako.

Ikiwa ungependa habari zaidi kuhusu uchunguzi wa utumbo, matiti au saratani ya mlango wa kizazi, tembelea

- cancersa.org.au
- breastscreen.sa.gov.au
- ncsr.gov.au

Ikiwa unahitaji msaada baada ya kugunduliwa na saratani, pigia simu **Cancer Council SA** kwa **13 11 20**.



Nyenzo hii iliundwa na Cancer Council SA na BreastScreen SA, kwa uchapishaji na utafsiri unaofadhiliwa na Country SA PHN.

Breast Screen SA

Government of South Australia
SA Health

phn COUNTRY SA
An Australian Government Initiative

Cancer Council SA

Kwa habari za bure* na za siri na usaidizi kuhusu saratani, Jumatatu hadi Ijumaa saa 3.00 asubuhi - 11.00 jioni (9am-5pm):

- pigia simu Cancer Council **13 11 20**
- zungumza kwenye mtandao **cancersa.org.au**
- tume barua pepe kwa **askanurse@cancersa.org.au**

Huduma ya bure* ya ukalimani inapatikana kwenye **131 450.**

*Gharama ya simu ya eneo

Ilipitiwa mnamo Februari 2025

Swahili | Kiswahili

Cancer Council SA

# Vipimo vya kugundua saratani mapema

## Taarifa kuhusu mipango ya uchunguzi wa saratani ya Australia



Utambuzi wa mapema wa saratani

Taarifa na msaada

**13 11 20**

**cancersa.org.au**




# Kugundua saratani ya utumbo mapema

Australia ina Mpango wa Kitaifa wa Uchunguzi wa Saratani ya Tumbo. Programu hutumia kipimo rahisi kupata dalili za mapema za saratani ya matumbo, mara nyingi kabla ya dalili kuonekana kwako. Kipimo kile kitatumwa nyumbani kwako.

Waaustralia wote wenye umri wa miaka 45 hadi 74 wanapaswa kufanya uchunguzi wa saratani ya matumbo kila baada ya miaka miwili.

**Umri wa miaka ya 45 hadi 49:** Agiza mtandaoni uchunguzi wako wa kwanza wa saratani ya utumbo. Baada ya hapo, utapata kipimo kipya kila baada ya miaka miwili moja kwa moja.

**Umri wa miaka ya 50 hadi 74:** Utatumiwa kipimo cha saratani ya matumbo kila baada ya miaka miwili bila kuhitaji kuagiza.

### Cancer Council SA inapendekeza:

- Kukamilisha na kurejesha seti yako ya kipimo inapofika kwenye posta.
- Kumwona daktari wako ikiwa una dalili za saratani ya matumbo. Dalili ni pamoja na kutokwa na damu kwenye puru yako, kuona damu kwenye choo au kwenye karatasi ya choo baada ya kutoa matumbo yako, kuvimbiwa au kuhara bila sababu, au uchovu usioelezeka.
- Kumwona daktari wako ikiwa una historia ya familia ya saratani ya matumbo.

**Changanua msimbo wa QR kwa:**

- **Kuagiza seti yako ya kwanza ya kipimo, au kipimo kingine.**
- **Tafuta habari katika lugha yako.**



# Kugundua saratani ya matiti mapema

BreastScreen SA inatoa uchunguzi wa bure wa mammogram ili kuweza kugundua saratani ya matiti mapema. Mammogram ni eksrai (x-ray) ya matiti.

Uchunguzi wa mammogram ni kwa wanawake wenye umri wa miaka 40 na zaidi, hasa wale wenye umri wa miaka 50 hadi 74.

Changanua msimbo wa QR au piga simu BreastScreen SA kwa nambari 13 20 50 ili uweke nafasi ya miadi ya mammogram yako bila malipo. Wanaweza kuweka miadi ya mkalimani wa kike kwa miadi yako bila gharama yoyote.

Wafanyakazi wote ni wanawake. Huhitaji rufaa kutoka kwa daktari wako ili kuhudhuria.

### Cancer Council SA na BreastScreen SA zinapendekeza:


- Kuwa na uchunguzi wa bure wa mammogram kila baada ya miaka miwili.
- Kujua mwonekano wa kawaida na hisia za matiti yako ili utambue mabadiliko yoyote. Mabadiliko ni pamoja na uvimbe, kutokwa na chuchu, au mabadiliko yoyote ambayo si ya kawaida kwako.
- Kuonana na daktari wako ikiwa unaona mabadiliko yoyote, kwani uchunguzi wa mammogram haufai kwako.

### Tembelea breastscreen.sa.gov.au:

- Kwa habari zaidi juu ya kufanya kipimo cha mammogram.
- Kwa habari katika lugha yako.

**Changanua msimbo wa QR kwa:**

- **Kuweka miadi yako ya mammogram mtandaoni.**



# Kugundua saratani ya shingo ya kizazi mapema

Kuchanjwa dhidi ya virusi vya papillomavirus vya binadamu (HPV) na kufanya kipimo cha mara kwa mara wa uchunguzi wa mlango wa kizazi kunaweza kukomesha saratani ya shingo ya kizazi.

Wanawake na watu walio na seviksi wenye umri wa miaka 25 hadi 74 wanapaswa kufanya uchunguzi kila baada ya miaka mitano kwenye kliniki ya matibabu. Unaweza kuchagua kufanya kipimo mwenyewe (kujikusanya), au daktari au muuguzi anaweza kukufanyia kipimo hicho.

### Cancer Council SA inapendekeza:

- Kuchanjwa dhidi ya HPV. Chanjo hiyo ni bure kwa watu wenye umri wa miaka 12 hadi 25. Pata chanjo kwenye duka la dawa au kliniki ya matibabu. Watoto katika Mwaka wa 7 wanapewa chanjo shuleni.
- Kufanya Kipimo cha Uchunguzi wa Kizazi kuanzia umri wa miaka 25.
- Unapofanya miadi yako, omba mkalimani ikiwa unamhitaji. Unaweza pia kuomba daktari au muuguzi wa kike ukipenda.
- Muone daktari wako kama una dalili zozote za saratani ya shingo ya kizazi. Dalili ni pamoja na kutokwa na damu katikati ya hedhi au maumivu wakati wa ngono.

**Changanua msimbo wa QR** kwa **maelezo zaidi kuhusu uchunguzi wa seviksi, ikiwa ni pamoja na chaguo la kujipima mwenyewe.**